

**OFISI YA RAISI**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA KOROGWE**

SHULE YA SEKONDARI MADAGO,

S.L.P 591,

KOROGWE.

TAREHE .....

SIMU:0712-039935/0655-608071

**KUMB.NA.MDGSS/JI/02/2021**

**JINA LA MWANAFUNZI .....**

**SHULE YA MSINGI ALIYOTOKA .....**

**S.L.P .....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA**

**SEKONDARI MADAGO MWAKA 2021**

**1.0** Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha .....  
Mwaka..... Hongera sana. Unatakiwa kufika shuleni tarehe .....  
Saa moja kamili asubuhi (1:00). Shule ya Sekondari Madago ipo Kata ya Makuyuni  
,Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe Km 1 kutoka barabara kuu itokayo Arusha/Moshi  
kwenda Tanga/Dar es salam. Muhula wa kwanza wa masomo utanza tarehe  
..... Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ..... na  
mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 Sare za Shule**

**Wavulana**

- a) Mashati mawili meupe(Tetron) yenye ukosi na mikono mifupi

- b) Suruali nyeusi mbili zenye mishono ya kawaida na zisiwe za kubana
- c) Mkanda mweusi wa ngozi (usiwe na bakozi kubwa)
- d) Tai nyeusi (rangi ya suruali)
- e) Viatu vyeusi vya ngozi (isiyopinduliwa ) vyenye kamba pea mbili
- f) Soksi nyeusi jozi mbili

### **Wasichana**

- a) Mashati mawili meupe (Tetron) yenye ukosi na mikono mifupi
- b) Sketi mbili za kijani
- c) Tai ya kijani( rangi ya sketi)
- d) Viatu vyeusi vyenye kamba pea mbili
- e) Soksi nyeupe jozi mbili ziwe ndefu

NB. Kwa wanaopenda kushona hijabu rangi ifanane na sare ya Shule,sketi iwe ndefu chini ya magoti

### **2.2. Vifaa vya kujifunzia**

- a) Daftari kubwa kubwa (counter book quire 3 zisizopungua kumi (10)
- b) Kalamu za kutosha (blue/black pen)
- c) Mkebe (mathematical set)
- d) Rula na penseli
- e) Begi la kuwekea daftari

### **3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

3.1 Shule inaandaliwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

### **3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule/Kusimamishwa shule**

- i. Wizi
- ii. Uasherati na ushoga
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi,cocaine,mirungi,kuberi n.k
- v. Utoro uliokithiri
- vi. Kupigana au kupiga
- vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- viii. Kudharau bendera ya Taifa
- ix. Kuoja au kuolewa
- x. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
- xi. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani ya shule au watu
- xii. Kuwa na simu ya mkononi
- xiii. Kukataa adhabu kwa makusudi

### **3.3. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni**

- i. Medical Examination form (Fomu) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- ii. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai (itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni)
- iii. Fomu ya mzazi kukiri /kukubaliana na sheria, kanuni ,taraatibu na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule (itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni)

**NB. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA MADAGO SEKONDARI**

.....

**MKUU WA SHULE**